Mchungaji Zaburi
(The Shepherd Psalm)

Zaburi 23:
na
Ellis P. Forsman

Mchungaji Zaburi
(The Shepherd Psalm)

Zaburi 23:

na

Ellis P. Forsman

Oktoba 5, 2011

Mchungaji Zaburi

Zaburi 23:

Zaidi ya karne 30 Zaburi 23 imesomwa, ikapendwa, na kukumbukwa na mamilioni ya watu. Maneno 180 ya Zaburi hii humuingia sana msikilizaji. Zinajieleza katika maelezo yanayoonekana ya uongozi, usalama, huruma, na baraka ambayo ni wale wamwitao Kristo Mchungaji wao.

Mtu wa mchungaji

Zaburi 23: 1, "*BWANA ndiye mchungaji wangu sitapungukiwa na kitu.*"

Bwana Mungu ndiye mchungaji wetu. Kwa Wakristo Kristo ndiye mchungaji wetu. Neno mchungaji linatuambia jinsi Mungu alivyo. Mchungaji anafahamika kwa ajili ya ukarimu wake, upole, na upendo unaojali. Zaburi 136 imejaa upendo mkuu wa Mungu.

Yesu alijawa na ukarimu na huruma; alisema katika Yohana 14:9, "*…Yesu akamwambia mimi nimekuwapo pamoja nanyi siku hizi zote, wewe usinijue, Filipo? Aliyeniona mimi amemwona Baba; basi wewe wasemaje, utuonyeshe Baba?*" Hivyo, tunavyomtazama Kristo tunamwona jinsi Baba (Mchungaji) alivyo. Tunapomtazama Baba tunamwona Kristo (Mchungaji) alivyo.

Yesu alisema, "*Mimi ni mchungaji mwema. Mchungaji mwema huutoa uhai wake kwa ajili ya kondoo.*" (Yohana 10:11). Alafu mistari ya 14-16 alisema, "*Mimi ndimi mchungaji mwema; nao walio wangu nawajua; nao walio wangu wanijua mimi; kama vile Baba anijuavyo, nami nimjuavyo Baba. Nami nautoa uhai wangu kwa ajili ya kondoo. Na kondoo wengine ninao, ambao si wa zizi hili; na haao nao imenipasa kuwaleta; na sauti yangu wataisikia; kisha kutakuwako kundi moja na mchungaji mmoja.*"

Hii haizungumzii Kanisa la Mashetani. Wanaddai kwamba kondoo halisi walikuwa ni Wakristo walioanzi Yerusalem kutoka katika siku ya Pentokoste, na hili kanisa la mashetani walikuwa ni kondoo wanaoongelewa kama "*sio wa kundi hili*". Kile ambacho kifungu hiki inaongelea walikuwa ni kondoo halisi ambao walikuwa ni Wayahudi, na Wakristo walikuwa ni kondoo ambao hawakuwa wa kundi hili.

Bwana ni "*Mchungaji **wangu***," alisema mtunzi wa zaburi. Mungu na Kristo siyo wanchungaji wa dunia; lakini wanavutiwa na kila mmoja. Kipindi cha Musa, Israeli walikuwa watu wa Mungu, na wakamtazama

ili awaongoze. Leo, wale walio wa ufalme wa Kristo ni watu wa Mungu. Toka siku ya Pentekoste wakati nafsi 3000 zilipoongezwa katika kanisa, idadi isiyosemwa ya watu wameweza kumuita Yesu "mchungaji wangu.

"*Sitapungukiwa*" (Kiyunani: "kutosheka"). Jukumu moja la msingi la mchungaji lilikuwa ni kutoa hitaji la kondoo. Kama mchungaji hana malisho mazuri kwa wao kuchunga, kondoo watataka kutafta malisho mazuri. Mistari ifuatayo inatuonyesha kuwa msaada wa Mungu kwa maitaji ya mwanadam:

Anafaham mahitaji yetu. Mat. 6:32-33, "*Kwa maana hayo yote mataifa huyatafuta; kwa sababu Baba yenu wa mbinguni anajua ya kuwa mnahitaji hayo yote. Bali utafuteni kwanza ufalme wake na haki yake; na hayo yote mtazidishiwa.*"

Anawapa wao waombao. Mat. 7:11, "*Basi ikiwa ninyi mlio waovu, mnajua kuwapa watoto wenu vipawa vyema, je si zaidi sana Baba yenu aliye mbinguni atawapa mema wao wamwombao?*"

Lakini siyo kama tukiomba kukosa. Yak. 4:3, "*Hata mwaomba wala hampati kwa sababu mwaomba vibaya, ili mvitumie kwa tamaa zenu.*"

Ikiwa tu tukiwa ndani yake. Yoh. 15:7, "*Ninyi mkikaa ndani yangu, na maneno yangu yakikaa ndani yenu, ombeni mtakalo lote nanyi mtatendewa.*"

Na hatawaacha wenye haki. Zab. 37:25, "*Nalikuwa kijana nami sasa ni mzee, lakini sijamwona mwenye haki ameachwa waala mzaao wake akiomba chakula.*"

Mahitaji yetu yatashughulikiwa. Fil. 4:19, "*Na Mungu wangu atawajazeni kila mnachokihitaji kwa kadiri ya utajiri wake, katika utukufu ndani ya Kristo Yesu.*"

Wakati mwingine kondoo anaweza kuwa katika malisho mazuri mno na asiridhike. Mchungaji wakati fulani akagundua kwamba kuna kondoo ambaye mara zote amekuwa akitafuta njia ya kupata malisho mengine ambayo ni zaidi ya ile waliomweka. Amekuwa akitoka nje, na mara akawaongoza wenzake wapotee, pia. Mchungaji alisema anapaswa kumwua ili kuwalinda kondoo wengine.

Wapo wale walioko katika kanisa ambao hawaridhiki na Kristo. Wanahitaji pia kitu chaa duniani. Biblia inatuambia hatuwezi kumfuata Mungu na mashetani. Mchungaji mwema anatujali. Hatupaswi kujali kile ambacho ulimwengu unatoa.

Kila zawadi njema tunayopokea hutoka kwa Baba yetu wa mbinguni. Yak. 1:17, "*Kila kutoa kuliko kwema, na kila kitolewacho kilicho kamili, hutoka juu, hushuka kwa Baba wa mianga; kwake haakuna kubadilika, wala kivuli cha kugeuka geuka.*"

Hakika, kila Mkristo anapaswa kusema, "*Sitapungukiwa.*"

Utoaji wa Mchungaji

Zaburi 23:2, "*Katika malisho ya majani mabichi hunilaza, kando ya maji ya utulivu huniongoza.*"

Kondoo huanza kuchunga saa 4:00 asubuhi, na wanaendelea kuchunga hadi katikati ya asubuhi, alafu wanalala chini. Kondoo hawalali chini kama wananjaa; wanalala chini ikiwa tu wameshiba. Kama wana njaa wataendelea kutafuta chakula.

Pia hawatalala chini kama wanaogopa au kutetemeka (kama vile adui au shinikizo). Kama mchungaji hayupo, kondoo watapigana (kama kuku walio na tabia ya kuumana; kondoo, kama wakiachwa, watatengeneza mapigano). Mchungaji mwema anawatia adabu kondoo wanaowachafua wengine.

Kondoo watakunywa maji baada ya kushiba chakula na vinginevyo. Lakini maranyingi hawako makini kuhusu ni maji gani wanapaswa kunywa. Wakiachwa wenyewe, watakunywa maji machafu, yaliyo na vijidudu. Mchungaji mwema anafaham maji haya, na kuwazuia kondoo wake wasiende pale kunywa, na badala yake anawapa maji masafi.

Kuna vinywaji vingi katika dunia hii ambayo ni hatari kwa Wakristo; na Mchungaji Mwema anatupa kinywaji kizuri. Kundi kubwa la watu duniani wana njaa na kiu ya kitu. Hawafahamu ni nini; hawapumziki. Kama tu watamruhusu Yesu awe Mchungaji wao, na kula neno la Mungu, watashibishwa kwa furaha. Watapata utulivu wa kiroho ambayo nafsi zao huililia sana.

Mat. 11:28-30, "*Njoni kwangu ninyi nyote msumbukao na wenye kulemewa na mizigo, nami nitawapumzisha. Jitieni nira yangu, mjifunze kwangu; kwa kuwa mimi ni mpole na mnyenyekevu wa moyo; nanyi mtapata raha nafsini mwenu; kwa maana nira yangu ni laini, na mzigo wangu ni mwepesi.*"

Njia iliyotolewa na mchungaji

Zaburi 23:3, "*Hunihuisha nafsi yangu; na kuniongoza katika njia za haki kwa ajili ya jina lake*."

Anahuisha vipi nafsi zetu? kondoo akipotea, anawatafuta na kuwaleta kundini. Kondoo akiugua, hawaachi wafe. Badala yake, anawabeba na kuwarudisha nyumbani, na kuwahudumia.

Yawezekana umewahi kusikia msemo usemao "poteza kondoo." Maana ni kwamba "wanaachiliwa chini" na hawawezi kusimama. Maranyingi kondoo akiwa amelala chini, anaweza kujiviringisha ardhini, na kulalia mgongo wake. Kwa wanyama wengi, hili sio tatizo;

wanajiviringisha na kusimama. Lakini kwa kondoo, hili ni tatizo. Uzito wao unawafanya wakijiviringisha wasirudi kawaida. Anaweza akafa haraka kama mchungaji asipomuwahi na kumgeuza.

Kondoo akijeruhiwa, mchungaji anawatibu majeraha. Yesu anawatibu wale ambao ni kondoo wenzetu katika kundi lake vivyo hivyo. Sikiliza maandiko haya:

Isa. 53:6, "*Sisi sote kama kondoo tumepotea; kila mmoja wetu amegeukiaa njia yake mwenyewe; na BWANA ameweka juu yake maovu yetu sisi sote.*"

Luka 19:10, "*Kwa kuwa Mwana wa Adamu alikuja kutafuta na kuokoa kile kilichopotea.*"

Tunapofanywa wagonjwa au kujeruhiwa na dhambi, Yesu atatoa dawa ya kiroho inayohitajika ili kuanza matibabu ya nafsi. Yak. 5:16, "*Ungameni dhambi zeenu ninyi kwa ninyi, na kuombeanaa mpate kuponywa. Kuomba kwake mwenye haki kwafaa aakiomba kwa bidii.*"

Angalia katika mustari wa 3 ya 23 Zaburi kwamba mchungaji ata "wao*ngoza*" kondoo wake katika njia ya haki. Mchungaji mwema atawaongoza kondoo wake kutoka katika malisho haya na kwenda katika lingine, mara nyingi, ili kuzuia malisho ya mahali pamoja. Kama malisho ni mabaya, kondoo wataharibu mizizi kwa kula karibu na ardhi. Mchungaji mwema atakuwa na mtiririko wa malisho anakopaswa kuwapeleka kondoo wake.

Mashariki, wachungaji hawawaendeshi kondoo wao. Wanawaongoza kwa sababu wanafahamu malisho ambayo wanataka wakachunge. Vivyo hivyo, Mungu hatatuendesha; atatuongoza kwenda pale tunakopaswa kuwa, kwa sababu anafahamu vyema. Yer. 10:23, "*…kuelekeza hatua zake si katika uwezo wa mwanadamu.*"

Sis, kama Wakristo, tunahitaji huongozi wa Kristo. Kondoo, wakiachwa wenyewe, watapotea. Hawana akili nzuri ya mwongozo; macho yao yana ukomo. Mit. 14:12, "*Iko njia ionekanayo kuwa sawa machoni pa mtu, lakini mwisho wake ni njia za mauti.*"

Uwepo wa mchungaji umehaidiwa kwa kondoo

Zaburib 23:4, "Naam, nijapopita kati ya bonde la uvuli wa mauti, sitaogopa mabaya; kwa maana wewe upo pamoja nami, gongo lako na fimbo yako vyanifariji."

Daudi alipofuga kondoo, "*bonde la uvuli wa mauti*" ilikuwa ni sehemu nyembamba kati ya milima miwili. Ilikuwa 4? urefu, urefu kwenda juu 1500, na umbali wa maili 10 hadi 12 upana wa chini. Mbwa mwitu walijificha walijificha kwenye vivuli, wakitafuta chakula, na walikuwa

tayari kuwarukia kondoo walipokuwa wanakuja. Kondoo hawakuogopa kwa sababu mchungaji alikuwepo pale kuwafukuza mbwa kwa fimbo yake. Fimbo ilitumika kama silaha ya kuwapigia wanyama wa mwituni, na kupiga vichaka ili waogope. Kifaa hicho kilitumiwa kwa kuwajali kondoo. Mchungaji angeweza kumshikilia kondoo kwa nguvu, akiangalia hali zao, au akiwatibu.

Tunapokumbana na hatari au nyakati za shida katika maisha yetu, nasi tunaweza kufarijiwa na mawazo kwamba Mchungaji wetu yupo kwa kutuongoza na kutulinda. Kuna bonde lingine ambalo wote tutakumbana nalo, siku moja. Nasi siku moja tutatembea kwa uhalisia kati ya bonde la uvuli wa MAUTI. Paulo alisema katika 1 Kor. 15:22, "*Kwa kuwa kama katika Adamu wote wanakufa, kadhalika na katika Kristo wote watahuishwa.*" Pia akasema katika Heb. 9:27, "*Na kama vile watu wanavyowekewa kufa mara moja, na baada ya kufa hukumu.*"

Wakristo hawaogopi kifo, kwa sababu wanajua Kristo atakuwa pamoja nao. Ufu. 1:17-18, "*Nami nilipomwona nalianguka miguuni pake kama mtu aliyekufa. Akaweka mkono wake wa kuume juu yangu, akisema, usiogope, mimi ni wa kwanza na wa mwisho, na aliye hai nami nalikuwa nimekufa, na tazama ni hai hata milele na milele. Nami ninazo funguo za mauti na za kuzimu.*"

Yesu aliharibu uchungu wa kifo kwa ajili yetu. "*Basi kwa kuwa watoto wameshiriki damu na mwili, yeye naye vivyo hivyo alishiriki yayo hayo, ili kwa njia ya mauti amharibu yeye aliyekuwa na nguvu za mauti, yaani ibilisi, awaache huru wale ambao kwamba maisha yao yote kwa hofu ya mauti walikuwa katika hali ya utumwa. Maana ni hakika hatwai asili ya malaika, ila atwaa asili ya mzao wa Ibrahimu.*" (Heb. 2:14-15).

Moja ya maneno yanayovutia katika Zaburi hii ni "*kati.*" Angalia kwamba tutapita "*kati*" ya bonde. Hatutakaa pale. Hii inamanisha kwamba hatutabaki kaburini, sehemu ya kusubiria. Kutakuwa na ufufuo. Yohana 11:25, "*Yesu akmwambia mimi ndimi huo ufufuo, na uzima. Yeye aniaminiye mimi, ajapokufa, atakuwa anaishi.*" 1 Kor. 15:57, "*Lakini Mungu na ashukuriwe atupaye kushinda kwa Bwana wetu Yesu Kristo.*"

Maandalizi yaliyofanywa na mchungaji

Zaburi 23:5-6, "*Waandaa meza mbele yangu, machoni pa watesi wangu. Umenipaka mafuta kichwani pangu, na kikombe change kinafurika. Hakika wema na fadhili zitanifuata sikuzote za maisha yangu; nami nitakaa nyumbani mwa BWANA milele.*"

Mchungaji "anaandaa meza mbele ya maadui zetu."

Nchi ya meza kwa kondoo ilikuwa ni mesa – ni sehemu tambarare iliyo nzuri kwa malisho kwenye milima. Mesa Kuu karibu na Delta, Colorado pia inafanana nah ii, isipokuwa ni kubwa sana. Mesa Kuu ni mesa kubwa duniani ikiwa na maziwa 300, na swala paa wengi na wanyama wengine wa mwituni. Kwa umbali, adui anaweza kuwaona kondoo wakila kama wakilindwa na mchungaji.

"Kumpaka mtu mafuta kichwani."

Kwa kondoo msemo huu ulikuwa ni kwa ssababu ya matibabu – zaidi kuwakinga na nzi na kupe, lakini pia kwa kuponya majeraha. Miili yao, isipokuwa kichwa, huzamishwa katika mafuta haya. Mafuta ya kichwa yalipakwa kwa mkono kwa makini. Mikoa tofauti ya dunia ilitumia mfumo tofauti kuliko mikoa mingine, lakini wote walitumia mafuta ya mbegu ya Lin na sulfur katika kuchanganyia.

Kwa wanadamu, kumpaka mtu mafuta kichwani ilifanywa kama tendo la kujipumzisha, na lilikuwa ni tendo la furaha. Mara nyingi hii ilikuwa ikifanywa na wageni au watu waliostahili heshima. Manukato yalijaa chumbani kwa harufu nzuri. Mwanamke mwenye dhambi katika Luka 7 alimpaka Yesu mafuta kichwani pake kwa manukato mazuri. Kwa kufanya hivyo alionyesha upendo wake kwa Kristo. Mungu ataleta furaha kwa kondoo wanaomfuata.

"Kikombe changu kinafurika."

Ilikuwa ni desturi kukijaza kikombe cha mgeni hadi kifurike. Daudi hapa, anaongelea baraka nyingi zinazokuja kwa wafuasi wa Mchungaji mwema.

Luka 6:38, "*Wapeni watu vitu nanyi mtapewa; kipimo cha kujaa na kushindiliwa na kusukwa sukwa hata kumwagika, ndicho watu watakachowapa vifuani mwenu. Kwa kuwa kipimo kilekile mpimacho ndicho mtakachopimiwa.*" Wema na fadhila katika kifungu vinawakilisha baraka za Mungu zinazosababisha kikombe kufurika.

"*Kukaa katika nyumba ya BWANA milele*" inaongelea makazi ya mbinguni kwa umilele.

Mat. 25:46, "*Na hao watakwenda zao kuingia katika adhabu ya milele; bali wenye haki watakwenda katika uzima wa milele.*" Yesu anaandaa sehemu kwa ajili yetu katika makazi ya Baba yake. Yohana 14:1-3, "*Msifadhaike mioyoni mwenu mnamwamini Mungu, niaminini na mimi. Nyumbani mwa Baba yangu mna makao mengi kama sivyo, ningaliwaambia; maana naenda kuwaandalia mahali. Basi mimi nikienda naa kuwaandalia mahali, nitakuja tena niwakaribishe kwangu; ili nilipo mimi nanyi mwepo.*" Ufu. 21:4, "*Naye atafuta kila chozi katika macho yao, wala mauti haitakuwapo tena, wala maombolezo, wala kilio; wala maumivu hayatakuwapo tena; kwa kuwa mambo ya kwanza yamekwisha kupita.*"

Je umewahi kuchota mchanga uliojaa ufuoni? Ni muda gani unadhani utachukua kuusambaza mchanga huo meza na kuuhesabu? Ni muda mrefu – ni muda mwingi mrefu kuliko unavyoweza kufikiria. Angalia ni muda gani utakuchukua kuhesabu idadi ya mchanga kwenye debe. Nadhani itakuchukua maisha yako yote. Sasa, angalia mchanga wote ulipo ufuoni katika dunia nzima. Fikiria tu, kama ungeishi zaidi kuweza kuhesabu mchanga mmoja mmoja ya ufuo wote ulimwenguni, kamaa ukimaliza umilele bado unaendelea!

Usipoteze wakati wako. Hakuna dhambi inayofaa kutumia wakati kama huo motoni.

Hitimisho

Mchungaji wetu (Mungu/Kristo) wanaweza kutupatia mahitaji yetu katika maisha haya, na katika maisha yajayo, lakini ili hili liwezekane ni lazima tuwe katika kundi lake.

Jinsi mtu anavyofanyika mmoja wa kundi lake? Mtu ni lazima afanyike Mkristo. Zifuatazo ni hatua muhimi zinazofanya hilo liwezekane:

- **Imani.** Waeb. 11:6, *"Lakini pasipo imani haiwezekani kumpendeza; kwa maana mtu amwendeaye Mungu lazima aamini kwamba yeye yuko, na kwamba huwapa dhawabu wale wamtafutao."* Nilipokuwa shuleni (nikiwa na miaka 17), kijana mmoja jirani yangu mwaka sawa na mimi akniambia kwamba haamini kwamba Mungu yuko. Kwa vile nilisha batizwa, nilichukua nafasi ya kuongea naye kuhusu mandiko. Akaniambia kwamba anaweza kuona kwamba kuishi maisha ya ukristo ni nzuri, lakini hakuwa na uhakika kwamba Mungu yuko. Lakini ili kuwa upande salama, labda anapaswa kwenda kanisani, na akifa na kusimama mbele za Mungu (kama kuna Mungu) siku ya hukumu (kama kuna hukumu), labda kama Mungu akiona kuwa amekwenda kanisani atampeleka mbinguni (kama kuna mbingu), na si motoni (kama kuna moto). Nikamwambia, "haifanyi kazi kwa njia hiyo. Lazima uamini katika yeye kwa moyo wako wote la sivyo huwezi kumpendeza.

- **Toba.** Matend. 2:38, *"Petro akawambia, tubuni mkabatizwe kila mmoja wenu kwa jina lake Yesu Kristo kwa ajili ya ondoleo la dhambi zenu nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu." Matend 11:18, "...Basi Mungu amewajalia hata mataifa nao <u>toba liletalo uzima."</u>* Kama ulikuwa unalala, ukasikia kelele kwenye chumba kingine, na unafikiria mwenyewe, "Kwamba kuna mwizi!" taratibu

unachukua simu ya mkononi, unawapigia polisi. Kidogo polisi wanafika na kumshika mwizi. Alafu anapiga kelele, "samahani; samahani!" Anaomba msamaha wa nini? Kwa sababu amekamatwa; si kwamba ameiba. Toba iliyokweli ni kwamba mwizi angeomba msamaha kwamba hataiba tena. Hiyo ndio toba ya kweli. Ni badiliko la nia linaloleta badiliko la matendo. Tunatakiwa kufanya hivyo kabla hatujawa wakristo.

- **Kukiri.** Waru. 10:9-10, *"Kwa sababu ukimkiri Yesu kwa kinywa chako ya kuwa ni Bwana na kuamini moyoni mwako ya kuwa Mungu alimfufua katika wafu, utaokoka. Kwa maana kwa moyo mtu huamini hata kupata haki, na kwa kinywa hukiri hata kupata wokovu."* Tuna kiri nini? Kwamba tuna amini kwamba Yesu Kristo ni mwana wa Mungu.

Kumbuka kwamba katika andiko hilo hapo juu kwamba imani (kuamini), toba, na kukiri ni "**KATIKA**" haki, uzima, au wokovu. "Katika" inamanisha kuelekeza kwenye kitu Fulani; si kwamba mtu ameshapata.

- **Ubatizo.** Ni katika ubatizo ndipo haki, uzima, na wokovu vinapatikana. Yesu mwenyewe alibatizwa kuitimiza haki yote, *"Lakini Yohana alitaka kumzuia akisema, mimi nahitaji kubatizwa na wewe, nawe waja kwangu? Yesu akajibu akamwambia kubali hivi sasa, kwa kuwa ndivyo itupasavyo kuitimiza haki yote. Basi akamkubali. Naye Yesu alipokwisha kubatizwa mara akapanda kutoka majini, na tazama mbingu zikamfunukia akamwona Roho wa Mungu akishuka kama hua, akija juu yake; na tazama sauti kutoka mbinguni ikisema, huyu ni mwanangu mpendwa, ninaye pendezwa naye."* (Math. 3:14-17). Yesu alibatizwa kwa sababu Mungu alisema ni jambo sahihi la kufanya. Unaona ni jinsi gani ilivyompendeza Mungu Yesu alipobatizwa? Yesu pia akasema, "*Imekuwa kwetu **sisi** kuitimiza haki yote."* Tuna batizwa kwa sababu inatimiza haki yake yote, si kwa sababu ni haki yetu.

Kwa kweli, tusipo batizwa, tungali katika dhambi zetu. *"Petro akawambia, tubuni mkabatizwe kila mmoja wenu kwa jina lake Yesu Kristo kwa ajili ya ondoleo la dhambi, na mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu."* (Matend. 2:38). Petro, umesema kusudi la ubatizo ni nini? "*Kwa ajili ya ondoleo la dhambi*". Kwa nini watu wanapenda kuach hatua inayotuondoa dhambi zetu?

Yesu aliamuru kwamba ili kuufikia wokovu lazima tubatizwe. *"Na akawambia enendeni ulimwenguni kote mkahubiri injili kwa kila kiumbe. Aaminiye **na** kubatizwa ataokoka; asiyeamini atahukumiwa."* (Marko 16:15-16).

Anania alimwambia Sauli (kabla hajaitwa Paulo) kitu iki hiki, "*Unakawilia nini? Simama, na ubatizwe, na uoshwe dhambi zako, ukiliitia jina la Bwana."* (Matend. 22:16). Ubatizo ni hitaji lililotolewa na Mungu.

Ubatizo unaitwa maziko, *"Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima."* (Waru. 6:4). Utu wetu wa kale umekufa. *"Hamfahamu ya kuwa sisi sote tuliobatizwa katika Kristo Yesu tulibatizwa katika mauti yake. Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake, kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima. Kwa maana kama mlvyounganika naye katika mfano wa mauti yake, kadhalika mtaunganika katika mfano wa kufufuka kwake; mkijua neno hili ya kuwa utuwetu wa kale ulisulubishwa pamoja naye, ili mwili wa dhambi ubatilike, tusiitumikie dhambi tena."* (Waru. 6:3-6). Ubatizo ni ramani ya Mungu inayotumiwa na damu ya Kristo katika maisha yetu kwa ubatizo. Tunakuwa huru na dhambi zetu za zamani kama tu tukibatizwa.

Hii haimanishi "kunyunyiza. Andiko hilo hapo juu linasema ubatizo ni maziko. Hatuwezi kupeleka maiti makaburini, na kumwekea udongo kidogo juu yake; tunauzika mwili.

Kama hujafanyika mshirika wa kundi la Kristo, kwa nini usizingatie leo?